336/1
LUGHA NA
FASIHI YA KISWAHILI
Paper 1
Oct./Nov. 2024
2 hours

# UGANDA NATIONAL EXAMINATIONS BOARD

## Uganda Certificate of Education

LUGHA NA FASIHI YA KISWAHILI

**Karatasi ya Kwanza**
(Uandishi wa Insha na Ufupisho)

Saa mbili

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA:**

*Karatasi hii ina sehemu* **mbili; A** *na* **B**. *Ina maswali matatu.*

*Jibu maswali* **mawili** *kwa ujumla ukichagua* **moja** *kutoka kila sehemu.*

*Swali la ziada halitasahihishwa.*

*Majibu* **yote** *yaandikwe kwenye kijitabu ulichopewa.*

*© 2024 Uganda National Examinations Board*

**Pindua**

CamScanner

## SEHEMU A

## UANDISHI WA INSHA

**Ama**

1. Mwenyekiti wa ngazi ya kwanza wa eneo lako aliitisha mkutano. Hii ilikuwa kwa sababu ya ukosefu wa usalama ambao ulikuwa umesababisha wasiwasi na uoga mwingi katika jamii. Wewe ni mmojawao wa waliohudhuria mkutano huo kama katibu.

   Andika yaliyojadiliwa.
   (*Tumia maneno kati ya* **220 - 250**)

**Au**

2. Kumekuwa na mashindano ya kandanda shuleni mwako na timu mbili zimefikia finali itakayochezwa kesho kutwa. Timu ya kidato cha tatu ina wachezaji hodari sana lakini timu ya kidato cha nne inasema liwe liwalo lazima waibuke washindi. Zawadi inayoshindaniwa ni ng'ombe dume na kombe la dhahabu. Mashabiki wa timu zote wamejitayarisha ifaavyo kugombana uwanjani kwa kila hali. Wewe ni kiranja mkuu shuleni na umeona ni bora uzungumze na wachezaji pamoja na mashabiki wao kabla ya finali yenyewe.

   Andika utakayowaambia ili wasilete fujo shuleni.
   (*Tumia maneno kati ya* **220 - 250**)

## SEHEMU B

## UFUPISHO

3. *Soma makala ifuatayo kisha uifupishe kwa maneno yasiyozidi* **themanini.**

### MADHARA YA DAWA ZA KULEVYA

Si jambo la kushangaza kwamba dawa za kulevya zina madhara chungu nzima. Ingawa ni vigumu kwa mtumiaji kutambua, matumizi ya dawa za kulevya yaweza kuhatarisha afya na hata kupunguza kipato chako na kusababisha umaskini. Madhara ya dawa za kulevya ni kama vile; madhara ya kiakili, madhara ya kiafya, ufujaji wa pesa, ni hatia kutumia baadhi ya dawa za kulevya, husababisha ajali au hata vifo na kadhalika.

Kwa kweli unaweza kuwa umeyasikia madhara haya au hata mengine mengi ambayo sijataja lakini je, unayajua madhara haya kwa kiasi gani? Kutambua madhara ya dawa za kulevya kunaweza kubadilisha maisha yako. Watu wengi wanaotumia dawa za kulevya hudhani dawa hizo hazina madhara yoyote kwa afya yao. Wao hudhani kuwa kutumia dawa ni kujiburudisha tu!



CamScanner

La hasha, huu ni uongo. Ukweli ni kwamba, yaelekea kuwa dawa zinaweza kuwa zinakufanya kujihisi vizuri lakini hatimaye zitadhuru afya yako.

Kabla hujafikiria kunywa chupa ya pombe, kuvuta sigara, bangi au kula miraa usisahau madhara haya hatari.

Dawa za kulevya huharibu akili ya mtumiaji. Hii ni kwa sababu dawa hizi hubadilisha namna mtu anavyofikiri na kumsababishia kusahau sana. Hata hivyo, mtumiaji sugu wa dawa hizi hujikuta katika hali ambapo hawezi kufanya jambo lolote bila kutumia dawa hizi.

Aidha, dawa za kulevya husababisha madhara ya kiafya. Dawa hizi huathiri takribani kila sehemu ya mwili kuanzia kwa moyo hadi maini. Matumizi ya dawa hizi husababisha magonjwa ya moyo, maini, figo na maradhi mengine mengi. Hata hivyo, ukiwa umelewa unaweza kukosa urazini na ukafanya ngono bila kinga na ukapata virusi vya UKIMWI. Kugawana sindano wakati wa kujichoma dawa hizo unaweza ukasababisha maradhi kama *hepatitis C* na *B*.

Ikumbukwe kuwa dawa za kulevya hazina madhara kwa afya ya mtumiaji tu pia ni hatia katika nchi yetu ya Uganda. Mtumiaji wa dawa hizi anaweza kufungwa jela akipatikana na hatia. Hata hivyo, baadhi ya makampuni kabla ya kukuajiri kwanza wanakulazimisha kupimwa ili kubaini ukiwa unatumia mihadarati. Kwa hiyo, uraibu wa mihadarati unaweza kukufanya kukosa ajira. Hata wachezaji hupimwa kwanza ili kubaini ikiwa wanatumia dawa za kusisimua misua.

Kadhalika, ukipatikana unaendesha gari baada ya kutumia dawa za kulevya unaweza kufungwa jela au kulipa faini kubwa.

Dawa za kulevya ni ghali mno, hivyo, ukizitumia kila mara utaishia kuwa maskini. Uraibu wa mihadarati pia huathiri utendakazi wako kazini au shuleni. Muda unaotumia kutafuta dawa hizo unaweza kuutumia kufanya mambo ya maana kazini au shuleni.

Ukitumia dawa za kulevya kuna uwezekano mkubwa wa kupata majeraha ya kimwili au kuhusika katika ajali ya barabarani. Pia, mihadarati inaweza kumfanya mtumiaji kujitia kitanzi. Visa hivi vya vifo vinavyohusiana na mihadarati vimeongezeka maradufu katika nchi nyingi duniani.

**Imetolewa**: New Vision, *Kiswahili Murua kwa Shule za Sekondari za Awali, Kidato cha Tatu*



**MWISHO**

CamScanner